SHEIKH MUHAMMAD KASSIM MAZRUI (1912-1982):

NAMNA ALIVYOUTUMIKIA UMMAH

KIMEANDIKWA NA:
GHALIB YUSUF TAMIM
(2018)

Sheikh Muhammad Kassim Mazrui (1912-1982) alitambulika kama Kadhi Mkuu wa Kenya (1 May 1963 – 30 April 1968), Mwanachuoni, *Mujaddid* (Mwana-mageuzi), Mwalimu wa Mashekhe na Ma-Kadhi kadha wa kadha, Mwandishi wa vitabu, Mhariri wa gazeti la *Sauti ya Haki* (1972-1982), na Swahibu na Mshauri Mkubwa wa Sh. Abdalla Swaleh Farsy (1912-1982).

Sh. Muhammad Kassim Mazrui alihudumu kama Kadhi wa Mombasa; Malindi; na Lamu (baina ya 1946-1963); na kama Kadhi Mkuu wa Kenya (1963-1968). Mbali na kazi za U-Kadhi, Sh. Muhammad alijishughulisha kuwafaidi Ummah kwa kuwaandikia vitabu vingi, na kuanzisha jarida la *Sauti ya Haki*, na kuiendeleza *Tafsiri ya Qur'ani* ilioanzishwa na Mwalimu wake, Sh. Al-Amin b. Ali Mazrui (1891-1947).

Kitabu hiki ni mahojiano baina ya Ustadh Uthman Naaman (Imam wa Msikiti wa Mazrui kwa zaidi ya miaka 20); Ghalib Yusuf Tamim (Mwandishi wa Maisha ya Ma-Ulamaa kadha wa kadha) na Al-Akh Abdalla Muhammad Awadh (Aliemtumikia Sh. Muhammad Kassim Mazrui katika kazi zake za Uwandishi baina ya 1980 hadi April 1982).

Majadiliano hayo yalifanyika katika Msikiti wa Mazrui, siku ya Jumapili tarehe 29 April 2018, yakinaswa kwa njia ya video na audio.

Ustadh Naaman ameanzisha mihadhara katika Msikiti wa Mazrui, Kibokoni, Mombasa, kuanzia 2011, akijaribu kuhuisha kumbukumbu za Ma-Ulamaa wetu walio jitolea kuutumikia U-Islamu.

Tunamuomba Allah awalipe Wanazuoni hao, Ustadh Naaman pamoja na Al-Akh Abdalla Muhammad Awadh kwa kazi zao. In shaa Allah, iwe ni *Sadaqatun Jariya* yao.

SHEIKH MUHAMMAD KASSIM MAZRUI (1912-1982): NAMNA ALIVYOUTUMIKIA UMMAH

KIMEANDIKWA NA:
GHALIB YUSUF TAMIM
(2018)

KITANGULIZI

Kitabu hiki juu ya *Sheikh Muhammad Kassim Mazrui (1912-1982): Namna Alivyoutumikia Ummah* ni cha tatu katika mfululizo wa vitabu alivyoandika ndugu yetu, Ghalib Yusuf Tamim, juu ya Wanavyuoni wa Afrika Mashariki waliozaliwa na kukulia Mombasa. Cha kwanza kilikuwa ni juu ya babu yake mwenyewe, yaani Sheikh Al-Amin bin Ali Mazrui. Cha pili ni kile cha *Maisha ya Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry (1850-1910 -* 1266-1372 H*)*. Na baina ya vitabu viwili hivi pia aliwahi kufanya utafiti na kuandika makala juu ya Sheikh Ali bin Abdallah Mazrui, babaake Sheikh Al-Amin. Mkusanyiko wa vitabu hivi ni tangizo muhimu katika maandishi tuliyo nayo kwa lugha ya Kiswahili.

Bila ya shaka kumetokea wengine waliotangulia kuandika makala juu ya baadhi ya mashekhe hawa, hasa juu ya Sheikh Al-Amin bin Ali Mazrui, na kwa kiwango kidogo zaidi juu ya Sheikh Muhammad Kassim Mazrui. Lakini sehemu kubwa sana ya maandishi haya imekuwa kwa lugha ya Kiingereza. Wanavyuoni wenyewe waliandika kwa Kiswahili kwa lengo la kunufaisha jumuiya zao. Lakini leo ikawa tarekh ya Wanavyuoni hawa haipatikani kwa ukamilifu ila kwa yule ajuae kusoma Kiingereza! Moto wa Uswahilini umetukuliwa kupalilia kuni za ilmu za Uzunguni. Kwa kuandika vitabu hivi kwa Kiswahili basi, Ghalib amefaulu kuifanya tarekh ya mashekhe hawa pia iwe ni katika makumbusho yetu

muhimu kwa lugha ambayo ni yetu na ambayo sote twaifahamu. Na kila vitabu hivi tukivisoma zaidi, ndivyo tarekh ya Wanavyuoni wetu itakavyozidi kuwa sehemu muhimu ya ukumbusho wetu wa pamoja – yaani *"collective memory."*

Mpaka sasa Ghalib ameandika juu ya mashekhe ambao ni wa ukoo wake mwenyewe. Yeye ni kitukuu cha Sheikh Ali bin Abdallah Mazrui na Sheikh Muhammad Kassim al-Maamiry. Sheikh Al-Amin bin Ali Mazrui naye alikuwa babu yake na Sheikh Muhammad Kassim Mazrui khali yake. Kwa upande mmoja, kuandika juu ya watu ambao ni wako ina changamoto zake, kwani wakisadifu kuwa na ila ya aina yoyote katika maisha au tabia zao huwa mwandishi aona taabu kuitangaza katika maandishi yake hata kama ila hiyo, ikiwa ipo kweli, haiwapunguzii utukufu wao kama Ma-Ulamaa wala kiwango cha heshima waliyo nayo machoni mwa watu wao. Hii ndiyo tabia yetu sote kama bianaadamu. Na kwa waandishi ambao ni Waislamu, kama Ghalib, kuna ile Hadith isemayo, "Tajeni mema ya maiti wenu na jiepusheni na kutaja mabaya yao" – kwani waliofariki hawawezi tena kujitetea. Kwa sababu mbili hizi – moja ya kibinaadamu na moja ya kidini – siku zote kuna hatari kuwa picha tutakayoipata ya yule mtu aliyeandikiwa kitabu na mtu wake itakuwa ni ya mraba mmoja.

Kwa upande mwengine, kuwa ni "mtu wa nyumbani" humpa mwandishi fursa kubwa ya

kujua mambo mengi ambayo si rahisi kwa mtu wa kando kuyajua. Alipotaka kuandika juu ya maisha ya Sheikh Al-Amin, kwa mfano, Ghalib alikuwa tayari ana ujuzi mkubwa wa mwanachuoni huyu uliotokana na kuishi pamoja na mmoja katika wakeze waliomkalia eda – yaani Bi Swafiya, nyanyaake Ghalib – na mwanawe mmoja – Bi Aisha, mamaake Ghalib. Hapo tena ilikuwa rahisi kwake kupata watu wengine, jamaa na marafiki – kama Maallim Saggaf Alawy – ambao waliweza kumpatia taarifa na maoni zaidi ya Sheikh Al-Amin. Shina la ujamaa wake na Sheikh Al-Amin sasa likapata mbolea kutoka kwa jamaa na ashabu wengine tungu nzima.

Katika kuandika kitabu juu ya Sheikh Muhammad Kassim Al-Maamiry, Ghalib pia hakutoka katika mipaka ya ukoo wake. Maamiry na Mazrui wa Mombasa ni ndugu kutokana na maingiliano na ndoa baina yao ya muda mrefu. Kutokana na uhusiano huu basi, Ghalib akaweza kupata kwa urahisi msaada mkubwa wa Salim Ahmad Muhsin Maamiry, na wengine aliowajulisha naye. Yaani kazi yake Ghalib ilirahisishwa kidogo kwa kuwa mmoja katika vitukuuu vya Sheikh Muhammad Kassim Al-Maamiry ni nduguye – udugu uliosaidia kumfungulia mlango wa tarekh hii.

Lakini katika hawa mashekhe wa ukoo wake hakuna ambaye Ghalib alimjua zaidi kwa nafsi yake kama Sheikh Muhammad Kassim Mazrui, kwani huyu peke yake ndiye aliyewahi kumuona na

kuingiliana naye mwenyewe kwa miaka mingi. Ghalib alibahatika kuwa miongoni mwa watoto wa Sheikh Muhammad kwani mmoja katika wake wa Sheikh Muhammad, Bi Salma Al-Amin, alikuwa ni khalati yake Ghalib, na watoto wa Bi Salma ni nduguze. Kwa hivyo siku zote aliweza kuingia na kutoka katika nyumba ya Sheikh Muhammad kama nyumbani kwao. Juu ya hayo, Ghalib aliishi na kulelewa na Shekh Muhammad na Bi Salma kwa kiasi cha miaka sita. Kwa hivyo ameweza kuiingilia mada hii ya maisha ya Sheikh Muhammad kwa "macho ya ndani," akimjua bwana huyu kwa vile alivyoishi maisha yake na kutokana na mazungumzo yao ya kawaida baina ya mwana na mzee wake.

Lakini Ghalib alifahamu kwamba ujuzi wake mkubwa wa Sheikh Muhammad Kassim Mazrui wahusu maisha yake ya kinyumbani, na kwa kiwango fulani maisha yake ya ukadhi tu. Ndipo alipoungana na Abdalla Muhammad Awadh ambaye, kwa maoni yake, alikuwa akijua mengi zaidi juu ya maisha ya Sheikh Muhammad kwa upande wa harakati na fikra zake za kitaaluma. Kama alivyoeleza Ghalib, Abdalla alipata bahati ya kufanya kazi kama "katibu" wa Sheikh Muhammad kwa kiasi cha robo cha maisha ya *Sauti ya Haki*, lile gazeti mashuhuri la Sheikh Muhammad Kassim Mazrui, na alipokuwa akitafsiri Qur'an. Basi Ghalib ameweza kuunganisha ule ujuzi wake wa kijumuiya na ujuzi wa Abdalla wa kitaaluma kuhusu maisha ya

Sheikh Muhammad, akatupatia kitabu hiki ambacho chatupa mwanga mzuri wa namna Sheikh Muhammad Kassim Mazrui alivyoutumikia Ummah wa Kiislamu hapa Afrika Mashariki.

Pengine baadhi ya wasomaji watastaajabu kuona kuwa Ghalib ametegemea maoni ya Abdalla tu, na hakuzungumza na nduguze wenyewe – kama kina Sheikh Munir na Sheikh Hammad – ambao bila ya shaka wana ujuzi wa ndani zaidi kuhusu kazi na fikra za Sheikh Muhammad kwa sababu walikuwa "makatibu" wa baba yao kwa muda mrefu zaidi kuliko Abdalla Muhammad Awadh. Lakini hili Ghalib alilifanya makusudi alipofahamu kwamba Sheikh Munir na Sheikh Hammad pia wamo katika harakati za kukusanya taarifa itakayosaidia katika kuandika kitabu juu ya baba yao. Kwa hivyo Ghalib hakupendelea kuingilia kazi ambayo tayari ilikuwa imeshaanzwa na nduguze, akaona afadhali ategemee kwengine katika kupata taarifa zaidi juu ya Sheikh Muhammad. Na kukitoka kitabu chengine juu ya Sheikh Muhammad basi, yamkini kitakuwa na taarifa nyengine ambazo ni tofauti na zile zilizomo humu, na mtazamo tofauti na ule uliojitokeza katika kitabu hiki. Na bila ya shaka, tofauti hizi za taarifa na mtazamo zina uzuri wake, kwani zitatusaidia kumwelewa Sheikh Muhammad tukipitia milango mbalimbali na kwa sababu hiyo tukaweza kuyaelewa maisha yake kwa ukamilifu zaidi.

Alipokata shauri kuandika juu ya Sheikh Muhammad Kassim Mazrui, Ghalib alifahamu kuwa huyu ni mmoja katika Wanavyuoni wakubwa wa Afrika Mashariki. Na kama mwalimu wake Sheikh Al-Amin, Sheikh Muhammad alikuwa mujaddid pia, akilenga kuleta mabadiliko muhimu katika utamaduni wa Kiislamu wa watu wa Afrika Mashariki. Ikiwa Sheikh Al-Amin ndiye aliyekuwa Mwanachuoni Mujaddid mkubwa wa nusu ya kwanza ya karne ya ishirini, Sheikh Muhammad alikuja kuwa mmoja katika Wanavyuoni Mujaddid wakubwa wa nusu ya pili ya karne ya ishirini. Moja katika natija muhimu ya kitabu hiki basi ni kule kuyadhibiti maendeleo ya historia ya kitaaluma miongoni mwa waislamu wa Afrika Mashariki takriban kwa karne nzima ya ishirini. Hapana shaka basi kwamba Ghalib astahiki kupongezwa vikubwa kwa maandishi yake muhimu aliyoweza kukamilisha mpaka sasa.

Alamin Mazrui,

Profesa, Chuo Kikuu cha Rutgers

Julai 12, 2018.

Sh. Muhammad Kassim Mazrui (1912-1982):

Mchango wake katika Mujtamaa

Utangulizi

Sheikh Muhammad Kassim Mazrui alitambulika kama Kadhi Mkuu wa Kenya (1 May 1963 – 30 Aprili 1968), Mwanachuoni, Mujaddid (Mwana-mageuzi), Mwalimu wa Mashekhe na Ma-Kadhi kadha wa kadha, Mwandishi wa vitabu, Mhariri wa gazeti la *Sauti ya Haki* (1972-1982 – 1392-1402 H), na Swahibu na Mshauri Mkubwa wa Sh. Abdalla Swaleh Farsy (1912-1982 - 1330-1402 H).

Sh. Muhammad Kassim Rashid Ali Naf'i Mazrui ni mzaliwa wa Mombasa katika mwezi wa Ramadhani 1330 Hijria, sawa na August 1912.

Sh. Muhammad Kassim alianza kusoma kwa Sh. Ahmad Muhammad Matano, na baadae kujiendeleza kwa Sh. Al-Amin b. Ali Mazrui (1891-1947 – 1308-1366 H) na kuwa mmoja katika wanafunzi wake wakubwa. Sh. Muhammad ndiye aliye zirithi kazi za Sh. Al-Amin. Alihudumu kama Kadhi wa Mombasa, Malindi, na Lamu.

Sh. Muhammad kwa kizazi anapatana na Sh. Al-Amin b. Ali Mazrui kwa Sh. Naf'i Mazrui, yeye akiwa ni **kitukuu cha Sh. Ali b. Naf'i Mazrui**, na Sh. Al-Amin akiwa ni **mjukuu wa Sh. Abdalla b. Naf'i Mazrui**. Hivi nikusema Sh. Al-Amin ni **Ammi** wa Sh. Muhammad.

Sh. Muhammad Kassim amezalika kutokana na vizazi vya Masheikh na Ma-Ulamaa, upande wa baba na mama. Babu yake upande wa baba, ni Sh. Rashid b. Ali b. Naf'i. Na mmoja katika babu zake upande wa mama ni Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry (1850-1910 – 1266-1372 H). Ma-babu hawa wote wawili walikuwa wanafunzi wa Sh. Ali b. Abdalla Naf'i (1825-1894 – 1240-1312 H). Mwalimu na wanafunzi wake wote wawili walihudumu kama Ma-Kadhi wa Mombasa:

— Sh. Ali b. Abdalla Naf'i alikuwa Kadhi wa Mombasa 1856-1870 (1272-1287 H)

— Sh. Rashid b. Ali Naf'i alikuwa Kadhi wa Mombasa 1870-1875 (1287-1292 H)

— Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry alikuwa Kadhi wa Mombasa 1875-1910 (1292-1372 H)

Nae Sh. Al-Amin pamoja na wanafunzi wake wawili pia walihudumu kama ma-Kadhi wa-Kuu:

— Sh. Al-Amin b. Ali Mazrui alikuwa Kadhi Mkuu wa Kenya 1937-1947 (1356-1366 H)
— Sh. Muhammad Kassim Mazrui alikuwa Kadhi Mkuu 1963-1968 (1362-1388 H)
— Sh. Abdalla Swaleh Farsy alikuwa Kadhi Mkuu 1968-1980 (1388-1400 H)

Profesa Alamin M. Mazrui ni mmoja katika wana wa Sh. Muhammad Kassim na Bi. Salma binti Sh.

Al-Amin Mazrui. Kwa heshima kubwa aliyokuwa nayo Sh. Muhammad juu ya Mlezi, Mwalimu na Mkwe wake huyu, alimtunukia mwanawe jina la Ammi yake huyu. Na siku zote anapomwita mwanawe, humwita kwa jina la **Ammi**! Kwa heshima ya Ammi yake, hakuwa akimkata mwanawe jina. Hichi ndicho kiegezo kimoja kwetu alicho tuachia Sh. Muhammad Kassim Mazrui tunapowapa wenetu majina ya wazee wetu.

Mwanawe mwengine ni Sh. Hammad Muhammad Kassim Mazrui, aliefuata khatua za babaake na kuwa Kadhi Mkuu wa Kenya (2002-2010 - 1423-1431 Hijria). Kabla ya hapo, Sh. Hammad alihudumu kama Kadhi wa Lamu (1992-1995 - 1412-1415 H) kama alivyokuwa babaake, na pia kuhudumu kama Kadhi wa Nairobi (1995-2002 - 1412-1423 H).

Sh. Muhammad amejifunza mengi kutoka kwa Sh. Al-Amin. Kazi hii ya uwandishi na uchapishaji ni moja katika yale aliyojifunza kutoka kwa Mwalimu wake huyu. Kwani Sh. Al-Amin alimpeleka Sh. Muhammad Kassim huko Zanzibar akajifunze namna ya kuitumia na kuirekibisha mashine ilokuwepo wakati huo ya kuchapisha ya *Cyclostyle*. Yeye pamoja na Mzee Haidar Bassamy wakawa ndio wachapishaji wa gazeti la *Sahifa* na *Al-Islah* aliyokuwa akiyaandika na kuyasambaza Sh. Al-Amin.

https://youtu.be/fFpQyMmFa68
https://youtu.be/SGd2ZKVaLlU
https://youtu.be/GB1x6NoEA5M

Kazi zake nyengine:

Sh. Muhammad Kassim Mazrui alifanya kazi ya Uwalimu kwa miaka mingi kabla ya kuchaguliwa kuwa Kadhi mwezi wa Julai 1946 (Shaaban 1365 H), akahudumu kama Kadhi wa Mombasa, Lamu na Malindi baina ya Julai 1946 (Shaaban 1365 H), na Aprili 1963 (Dhul Hijja 1382 H). Hapo tena akachaguliwa rasmi kuhudumu kama Kadhi Mkuu wa Kenya kuanzia tarehe 1 May 1963 (7 Dhul Hijja 1382 H) hadi 30 Aprili 1968 (2 Safar 1388 H). Baada ya kuhudumu kwa muda wa miaka mitano, Sh. Muhammad akjiuzulu kwa sababu za kiafya. Serikali ya Kenya ikamchagua rafiki na Mwanafunzi-mwenza, Sh. Abdalla Swaleh Farsy kuichukua nafasi hiyo ya Kadhi Mkuu. Ma-Ulamaa wawili hawa waliweza kuiendeleza kazi za Mwalimu wao, Sh. Al-Amin b. Ali Mazrui za kusomesha, kuandika na pia kazi za Kadhi Mkuu wa Kenya – Alhamdu Lillah! Allah awabariki Ma-Ulamaa watatu hawa na awalipe malipo mema ya Jannatul Firdaus, In shaa Allah.

Sh. Muhammad alikuwa akisomesha Darsa katika kila mji aloutumikia kama Kadhi:

1. Kadhi/Mombasa
2. Kadhi/Malindi
3. Kadhi/Lamu
4. Alishikilia kiti cha Kadhi Mkuu wa muda mara kwa mara kuanzia 1950 (1369 H) pale

alipojiuzulu Sayyid Ali Badawy (1903-1987 – 1321-1407 H)

5. May 1, 1963 (7 Dhul Hijja 1382) akachaguliwa rasmi kuwa Kadhi Mkuu wa Kenya mpaka alipostaafu mwisho wa April 1968 (2 Safar 1388). Serikali ya Ukoloni ilifurahishwa sana na uhodari wa kazi yake na heshima kubwa aliyokuwa nayo. Kwa hivyo wakati Sh. Muhammad Kassim alipopendekezwa kuwa Kadhi Mkuu na Liwali Bw. Salim Muhashamy (1911-1979 – 1329-1399 H), hawakuwa na tashwishi tena ila kumkubali.
6. Aliweka Darsa maalum za Wazee katika Msikiti wa Mazrui. Na wale walopendelea somo maalum, aliwawekea nafasi yao nyumbani kwake. Sh. Ali Darani na Sh. Ali Mwenzagu, kila mmoja wao aliwekewa wakati wake maalumu kusoma elimu ya Ukadhi.
7. Aliwawekea kina mama Darsa yao maalum katika Msikiti wa Al-Azhar, Baghani, Mombasa, ili na wao waifahamu dini yao vilivyo.

Kwa ujumla Sh. Muhammad Kassim amehudumu kama Kadhi/Kadhi Mkuu kuanzia July 1946 (1365 H) hadi April 1968 (1388 H) – muda wa miaka 22.

Sh. Muhammad Kassim Mazrui alifariki tarehe 5 April, 1982 (10 Jumadal Akhira 1402 H), na kuzikwa katika Makaburi ya Mazrui yaliopo

mkabala na Ngomeni na Mombasa Club, Kibokoni, Mombasa. Aliswaliwa Msikiti wa Mandhry baadal Asri. Aliyeiongoza swala ya maiti ni mwanawe mwenyewe, Bw. Munir Muhammad Kassim. Hapo tena jeneza lake likachukuliwa kwa heshima na masikitiko makubwa na ummati mkubwa uliohudhuria mazishi ya Ulamaa huyu. Maiti ya Sh. Muhammad ikateremshwa katika mapumziko yake ya *Barzakh. Inna Lillahi wa inna Ilaihi rajiuun* – Kwa hakika sote twatoka kwa Allah, na Kwake Yeye ndio marejeo yetu. Tunamuombea malazi mema, na, In shaa Allah, aipate Jannatul Firdaus kwa kazi yake kubwa ya kuutumikia Ummah.

UWANDISHI WA Sh. Muhammad Kassim Mazrui

Kitabu hiki ni mahojiano baina ya Ustadh Uthman Naaman (Imam wa Msikiti wa Mazrui kwa zaidi ya miaka 20); Ghalib Yusuf Tamim (Mwandishi wa maisha ya Ma-Ulamaa kadha wa kadha, akiwemo Sh. Al-Amin b. Ali Mazrui, Sh. Ali b. Abdalla Naf'i na Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry); na Al-Akh Abdalla Muhammad Awadh (aliyemtumikia Sh. Muhammad Kassim Mazrui katika kazi zake za Uwandishi).

Yafuatayo ndio masuali tuliomuuliza Al-Akh Abdalla Muhammad Awadh:

Assalamu Alaikum wa Rahmatu Llahi wa Barakatuhu.

1. Sh. ABDALLA! Tumefurahi sana kwa kuitikia uwalishi wetu ili utupe ufahamu wako juu ya kazi alizozifanya Sh. Muhammad Kassim Mazrui.

2. Tungependa kwanza ujitambulishe kwa wasikilizaji wetu

- Jina lako kamili, na mahusiano yako na Sh. Muhammad Kassim.

3. Alhamdu Lillah! Sh. Muhammad Kassim anajulikana kama Ulamaa, Kadhi Mkuu wa Kenya, Mwandishi, na Mwalimu wa Mashekhe.

4. Wewe ulimpata Sh. Muhammad Kassim katika wakati gani wa maisha yake?

5. Ni maandishi ya aina gani yalokuwa yakimshughulisha Sh. Muhammad Kassim?

6. Ni changamoto gani alizokumbana nazo katika uwandishi wake?

7. Nini lilokuwa kusudio lake katika kuandika kwake?

8. Jee ni vitabu gani alivyoandika? - Tafadhali tutajie majina ya vitabu alivyoandika.

9. Sh. Muhammad Kassim pia alikuwa na gazeti alikuwa akichapisha. Tutajie jina la gazeti hilo, na tueleze kwa ufupi kusudio la gazeti hilo, na likiwafikia kina nani, na likiwafikia vipi?

10. Nini mchango wako katika uwandishi huu, ulijihusisha vipi au ulihusishwa vipi?

11. Jee walikuwepo wengine mlokuwa mkisaidiana nao katika kazi hii. Mulisaidiana vipi katika kazi hii ngumu?

12. Mbali na vitabu na gazeti, Sh. Muhammad Kassim aliiendeleza Tafsiri ya Qur'ani ya Mwalimu wake, Sh. Al-Amin bin Ali Mazrui. Jee uwandishi huu ulichukuwa mwelekeo gani?

13. Kwa sababu ya kundeleza kazi hizo za Sh. Al-Amin, tutajie msimamo wake juu ya Sh. Al-Amin. Na nini mahusiano ya hawa Mashekhe wawili?

14. Sh. Muhammad Kassim alisifika kwa uhodari wa mashairi, jee una kumbukumbu zozote juu ya mashairi yake?

15. Sh. Muhammad Kassim Mazrui na Sh. Abdalla Swaleh Farsy walikuwa marafiki wakubwa. Mmoja akampokea mwenziwe katika kazi za Kadhi Mkuu wa Kenya. Tupe uliyoyaona wewe katika urafiki wao huu. Nini yalokuathiri wewe, au ulichokisoma katika urafiki wa Ma-Ulamaa wawili hawa.

16. Jee ungependelea tujifunze nini kutoka kwako kwa nafasi tunu uloipata ya kumtumikia Sh. Muhammad Kassim Mazrui katika kazi yake ya kuutumikia Mujtamaa wetu?

Haya yafuatayo yatokana na majibu ya Abdalla Muhammad Awadh na baadhi ya vijalizo vya Mwandishi kulingana na utafiti Zaidi aloufanya:

KITAMBULISHO CHA ABDALLA

Abdalla Muhammad Awadh (Mzaliwa wa Takaungu, mwaka wa 1956 – sawa na 1375 H) ni nduguye Maalim Khamis Omar Mazrui – mama zao ni ndugu. Mamaake Abdalla ni Bi. Sanura binti Salim b. Rashid Mazrui; nae mamaake Maalim Khamis ni Bi. Fadhila bint Salim b. Rashid Mazrui. Maalim Khamis amemuoa binti wa Sh. Muhammad Kassim, Bibi Maimuna. Hawa ni wazazi wa Muhammad Khamis (M. K. Mazrui), Nabila na Najda Khamis Mazrui. Abdalla amelelewa na khalati yake, mamaake Maalim Khamis, kutoka akiwa na umri wa mwaka mmoja unusu. Alipomaliza masomo yake ya shule ya msingi huko Takaungu, alichukuliwa na Maalim Khamis na Dada Maimuna ili aweze kuendelea na masomo ya shule ya upili mjini Mombasa. Na kwa sababu ya walezi wake hawa akapata bahati ya kukulia pia katika nyumba ya Sh. Muhammad Kassim.

Baada ya Abdalla kumaliza kidato cha nne na kuanza kazi, aliombwa na Al-Akh Munir Muhammad Kassim Mazrui (wa MUHURI), kakaake Bi. Maimuna, pale anapowasiika, amsaidie Sh. Muhammad katika kazi zake za uwandishi. Na Alhamdu Lillah, Abdalla akapata bahati ya kuwa karibu sana na Sh, Muhammad kuanzia mwaka wa

1979 (1399) hadi April 1982 (Jumadal Akhira 1402), takriban miaka miwili unusu. Sheikh na mjukuu/msaidizi wake huyu wakawa wapo pamoja kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa kila wiki kwa muda wa masaa matatu kila siku, katika mazingira ya utulivu wa shamba, Kisauni.

Tunu hii aloipata Abdalla Muhammad Awadh miaka 39 ilopita ndio ilio tupelekea kumuomba atufaidishe na sisi. Kwani kila saa moja unayo tumia kukaa na Mwanachuoni ni Madrasa tosha, siuze masaa takriban 1620 (*masaa 3* x *siku 5 kila wiki* x *4 kila mwezi* x *miezi 27*), aloyapata Abdalla kukaa ana-kwa-ana na Sh. Muhammad Kassim Mazrui katika kuzichambua Tafsiri mbali mbali, huku wakiyanakili kwa njia ya maandishi ili yawafikie Ummah.

Majadiliano yetu yalichukua takriban masaa mawili katika Msikiti wa Mazrui, siku ya Jumapili tarehe 29 April 2018 (13 Shaban 1439 H). Majadiliano yakinaswa kwa njia ya video na vinasa sauti vya simu ya rununu.

Makutano baina ya Sh. Muhammad Kassim Mazrui na Bw. Abdalla Muhammad Awadh

Sh. Muhammad alistaafu kama Kadhi Mkuu wa Kenya 30 April 1968 (2 Safar 1388) na kufariki tarehe 5 April 1982 (10 Jumadal Akhira 1402) – miaka 14 kama Mstaafu (*Retiree*). Alistaafu kazi ya Serikali na kujishughulisha na kazi za kuutumikia Ummah kwa njia nyengine mbali mbali. Na kazi

kubwa ilikuwa ni kazi ya uwandishi juu ya kuwa hali yake ya kiafya haikuwa nzuri hivyo. Alikuwa na matatizo ya macho na kuhangaishwa na pumu.

Alhamdu Lillah! Katika miaka hii 14 aliitumia kuandika vitabu, makala na jarida la *Sauti ya Haki* na Tafsiri ya Qur'ani. Akaweka Darsa mbali mbali, nyengine zikiwa nyumbani kwake, na nyengine Msikitini. Akawa Mshauri wa wengi, mmoja wao akiwa Sh. Abdalla Swaleh Farsy. Abdalla alimtumikia Sh. Muhammad katika miaka yake miwili unusu ya mwisho (1980-1982). Walokuwa wakimsaidia katika uwandishi kabla ya hapo ni wanawe. Al-Akh Munir Muhammad Kassim alijitahidi sana kumpa babaake motisha na usaidizi wa kila alichokihitaji Sh. Muhammad katika kuitimiza azma yake ya kuandika vitabu, majarida na Tafsiri ya Qur'an.

Sh. Muhammad alitia nia ya kuandika wakati atakapostaafu kazi za Ukadhi na Ukadhi Mkuu. Lakini pale alipostaafu, hali yake ya kiafya haikuwa nzuri. Ikawa anaungulika kujiona kuwa yale aloyakusudia anashindwa kuyatimiza. Bw. Munir pamoja na nduguze wakawa wanamshawishi baba yao asisikitike. Wakamhakikishia kuwa watasimama nae kidete wamsaidie kwa kila hali ili aweze kuitimiza ndoto hio.

Bw. Munir akasimama kwa hali na mali, yeye pamoja na nduguze, mpaka Sh. Muhammad akakinai kuwa sasa aweza kuitimiza azma yake.

Hapo tena akaisahau hali yake ya kiafya, akamakinika na kujishughulisha. Alhamdu Lillah yakapatikana mazao mengi. Utaalamu na ufahamu wake wa kidini na kimaisha ukadhihirika kwa kazi kubwa aloifanya katika kuutumikia zaidi Ummah.

Heko kwa Bw. Munir Mazrui pamoja na nduguze kwa kuifufua ndoto na azma ya baba yao, mpaka zikapatikana lulu na marjani. Alhamdu Lillah! Allah akawatilia Tawfiki. Na, In shaa Allah, watanali saada kwa kazi kubwa walioifanya – Amin.

Kipindi alichokiwahi Abdalla, ni kipindi ambacho Sh. Muhammad na yeye waliweza kutumia muda mrefu zaidi kila siku katika kazi hii ya uwandishi. Na kazi ya uwandishi ni kazi pevu, kwani inakubidi uchambue vitabu mbali mbali, na kuyatathmini maandishi hayo. Na pia inahitaji kuwahoji watu tofauti tofauti kutegemea mada unayo iandika. Kwa hivyo ni kazi inayo hitajia ujuzi, utulivu, umakinifu na hekima kubwa.

Alhamdu Lillah, Abdalla alipata bahati kubwa ya kupokea na kunakili mengi kutoka kwa Sh. Muhammad.

Maandishi yalokuwa yakimshughulisha Sh. Muhammad Kassim Mazrui

Sh. Muhammad alikuwa akiyafuatilia mambo yanayo jitokeza katika mujtamaa kila leo. Na mifano mizuri yaliyojitokeza wakati alipostaafu ni safari ya kwenda na kutua mwezini, mambo ya

kupanga uzazi, uraibu wa marungi, uchinjaji wa n'gombe - kwanza kwa kupigwa *stenn-gun*, n.k. Na kila kinachojitokeza, kinacho hitaji kufafanuliwa, alikuwa akiyaandika na kuwawekea wazi Ummah katika Makala mbali mbali na pia katika jarida lake la *Sauti ya Haki* au kuwaandikia kitabu.

Changamoto alizokumbana nazo Sh. Muhammad katika uwandishi wake

Unapojitolea kuamrisha mema na kukataza maovu, basi ni lazima utapata marafiki na maadui, wafuasi na wapinzani. Na ndio maana Allah katika Surah Al-Asr anasema:



Al-Asr (103): *Kwa Jina la Mwenye-ezi-Mngu, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu. Naapa kwa zama. Hakika binaadamu bila shaka yumo katika khasara. Ila wale walioamini na wakatenda mema,* ***na wakausiana kwa haki, na wakausiana kusubiri.***

Ukisha chukua jukumu la kuwausia watu juu ya haki, basi uwe tayari kusubiri kwa yale yatakayo kupata. Kwani ni tabia ya binadamu kuipinga haki, hasa ikiwa haki hiyo inamuharibia starehe yake au pato lake. Kwa hivyo changamoto kubwa ilikuwa ni

lawama na upinzani kutoka kwa wale ambao hawakuifurahia kazi hii ya Sh. Muhammad, hasa wale walokuwa wakiyapenda mambo ya bid'a na ya upotofu. Na wengi walikuwa wakipinga sio kwa sababu hawaijui haki, bali upinzani wao ni kwa nini jambo hilo lisemwe na Sh. Muhammad Kassim. Na upinzani wa aina hii unaelemea zaidi upande wa hasadi.

Mifano:

1. **Uchinjaji n'gombe kwa kutumia bunduki ya *Stenn-gun***

Mfano mzuri ni ule upinzani ulojitokeza 1969 wakati Shirika la Uchinjaji *Kenya Meat Commission* (KMC) lilipoanza kutumia bunduki ya *Stenn-gun* ili kuwavunja nguvu n'gombe kabla ya kuchinjwa. Kwa sababu ya idadi ya n'gombe wanaochinjwa kwa siku, na shida ya kupigana nao kabla ya kuchinjwa, ilipatikana njia rahisi ya kumvunja nguvu yule n'gombe kwa kumpiga bunduki na kumtoa fahamu. Akianguka huwahiwa na kuchinjwa. Wengi wakadhani kuwa nyama hiyo haitakuwa halali kuliwa. Pakahitajika ufafanuzi kutoka kwa viongozi wa Dini.

Sh. Muhammad kabla ya kutoa fatwa ya uhalali au uharamu wa njia hiyo, akataka apelekwe KMC akajionee mwenyewe kila kinacho fanyika wakati wa uchinjaji n'gombe. Akapelekwa na kushuhudia kila mbinu inayo tumiwa. Akajadiliana na wafanyi kazi wa KMC na baada ya kutosheka kuwa ile

bunduki anayo pigiwa n'gombe si ya kumuua, bali ni ya kumvunja nguvu. Na pia anapochinjwa, damu inatoka kama inavyo takiwa na kukubalika na sharia. Baada ya kukinai, ndipo alipotoa fatwa ya kuwa uchinjaji huo unakubalika kisharia na nyama ya n'gombe hao ni halali kuliwa. Hapo tena ulobaki ukawa ni upinzani usiokuwa na nguvu. Ummah ukaridhika na kufaidika na fatwa ya Sh. Muhammad Kassim. Ikumbukwe kuwa tukio hili ni kabla ya kuanzishwa jarida la *Sauti ya Haki*.

2. Uraibu wa Marungi

Uraibu huu unatumika sana katika miji ya Wa-Islamu. Pamekuwa na mijadala mengi juu ya uhalali na uharamu wake. Inahitaji utafiti na uchambuzi wa kina kabla ya kuhalalisha au kuharamisha. Zipatikane hoja za kukinaisha kabla ya kutoa uamuzi.

Kwa sababu Sh. Muhammad Kassim hakupenda kusema jambo bila ya ithbati kamili, alifanya utafiti juu ya majani haya ya marungi yanayo changamkiwa na wengi. Ni uraibu unaopendwa na wengi, na ni biashara kubwa kwa wauzaji waliojikita katikati ya miji na mitaa ya Wa-Islamu – jina lao maarufu, *Kwa Mmeru*.

Sh. Muhammad aliwaita watumiaji sugu wa mairungi na kuwahoji kila mmoja kwa utaratibu wa Mtafiti Shupavu. Ikawa kila mmoja anaitwa kwa wakati wake, ili pasiwe na pazia au kusaidiana kwa maoni. Kila mmoja akatakiwa ajieleze ameyatumia

mairungi kwa muda gani; ni faida au hasara gani anazozipata; nini hisia zake kabla ya kula na baada ya kuyala mairungi. Na nini maoni yake yeye mwenyewe yule mtumiaji baada ya utumiaji wa muda mrefu. Na kwa vile ameshakuwa mraibu, nini wasia wake kwa wale ambao hawajaanza kutumia uraibu huo.

Haya ni baadhi ya majibu yalio tolewa:

- Marungi yanavunja nguvu za kiume na kusababisha kuvujwa maji ya uzazi bila kujifahamu.
- Hurusha na kupoteza usingizi. Huweza kukupelekea kuharibu akili na kuwa mwandazimu.
- Handas zikisha panda huanza kujenga majumba hewani.
- Uraibu unakupelekea kuwa mbadhirifu na ikawa kila uanchokipata chenda katika starehe hiyo.
- Inaharibu meno na maida.
- Baadhi yao wamefanyiwa upasuaji mara kadha na kutolewa uchafu ulojikusanya matumboni.

Baada ya kujadiliana na waraibu hao, akawaita baadhi ya madaktari wa hospitali ya wandawazimu ya Port Reitz, Mombasa, hasa wale madaktari wa Ki-Islamu walowauguza waraibu wa mairungi.

Sh. Muhammad baada ya utafiti wa kina na kukinai hasara kubwa zinazo patikana kutokana na uraibu

huu, ndipo alipotoa fatwa ya kuyaharamisha marungi. Akatoa maelezo marefu na pia kumpa daktari mmoja atie Makala yake katika *Sauti ya Haki* – (angalia Hukumu ya Qaat – Miraa – Marungi, katika SYH Vol II, March 1975, Safar 1395, Ukurasa wa 7).

Huu ndio ulokuwa uhodari wa Sh. Muhammad Kassim – Mwanachuoni Mtafiti. Na hivi ndivyo anavyoeleza Profesa Issa Shivji wa Tanzania, *"Moja katika sifa za Mwanachuoni ni kusema na kueneza ukweli unaotokana na utafiti, uchambuzi na uelewa wake kwa jamii bila ya kujali kama ukweli huo unawapendeza au unawaudhi baadhi ya watu au watu wote."*

Kusudio lake katika kuandika

Matatizo makubwa yaliyo kuwepo wakati huo ni udhaifu wakuufahamu U-Islamu na itikadi potofu zilizotiwa katika Dini.

Mujtamaa ulikuwa umetawalia na watu ambao walipenda kuutumia udhaifu huo ili wajifaidi wenyewe. Wakapenda kuuelemaza Ummah na kuwawacha watu katika ujinga. Ikawa mambo kama ya bid'a na karama ndiyo yalowekwa mbele na kuyafanya kuwa ndiyo mambo muhimu katika Dini.

Kama Ulamaa akaona amewajibika kuwazindua ndugu zake ili waifahamu dini yao na watoke katika unyonge wakutawaliwa na kugandamizwa na watu wachache.

Kwa hivyo Sh. Muhammad akajitahidi kuyaweka wazi mafunzo ya Ki-Islamu ili watu waijue dini yao inawaamrisha nini na kuwakataza mambo gani. Akaingia katika kazi ya kuwaandikia majarida na vitabu vya kuwafafanulia kila jambo lililokuwa likiwatatiza. Kwa hivyo maudhui mengi yakawa ni juu ya mambo yalokuwa yakijitokeza na kuwatatiza Ummah. Mifano ya uwandishi wake ni jarida la *Sauti ya Haki* na vitabu juu ya *Hukumu za Sharia*.

Tukinukuu baadhi ya malengo alokuwa nayo katika uandishi wake kutoka kwa *Sauti ya Haki*, toleo No. 2/82 la 1 May 1982 (6 Rajab 1402):

Kila Islamu ajua kuwa baada ya nguzo za dini, jambo muhimu ni Imani. Na Mtume Muhammad (S.A.W.) ametuwekea vipimo ili kila Islamu ajue kadri ya Imani yake katika dini. Lakini si jambo la nadra katika Ummah wetu kuona taasubi na ujinga katika kuamini kwetu – kuona watu wakijitolea kwa hali na mali kupigania jambo waliaminilo, ingawa pengine jambo hilo tukilitaili tutaona haliingii katika mipaka ya dini. Na hapa ndipo tuwezapo kufahamu umuhimu wa al-marhum (Sh. Muhammad Kassim Mazrui) kwa Ummah wa Islamu wa hapa kwetu. Kwani al-marhum alikuwa hatosheki na Imani tu. Alikuwa akisisitiza kuwa jambo limtafautishalo binadamu na mnyama ni akili. Mwenye-ezi-Mngu Amemtunukia binadamu akili na mantiki ya kupima matendo na Imani ya jumuiya yake, kwa mujibu wa msingi wa mafunzo ya dini ya

Kiislamu. Alikuwa akisisitiza kuwa Imani tupu isiyoongozwa na akili mantiki na ufahamu mwema ni Imani iwezayo kupotoka na kuporomoka kwa wepesi sana; kwamba kutoipalilia Imani kwa akili tuliyopawa na Mwenye-ezi-Mngu ni kwenda kinyume na maumbile ya binadamu. Kwa ufupi kwamba msingi thabiti wa Imani upo katika kuifikiria Imani hiyo na kuifahamu kwa nadhari ya mantiki.

Kwa kufuata nyayo za wataalamu kama Sheikh Al-Amin bin Ali, Sheikh Ali bin Abdalla na wengineo, basi al-marhum Sheikh Muhammad Kassim Mazrui alikuwa na lengo la kuleta mapinduzi ya fikra katika jumuiya yake, mapinduzi yatakayo wakomboa watu na pingu za ujinga na taasubi zilizowakabili ili wajibidiishe kuleta mabadiliko yatakayo oana na njia ya haki,

Katika uwandishi wake alijitahidi kuwahusisha wataalamu mbali mbali, ili na wao pia wapate nafasi ya kutoa michango yao ya kuwanufaisha watu kwa ule utaalamu wao. Ma-Profesa Muhammad Hyder (Mtaalamu wa *Zoology),* Abdalla Naji *Said (Mtaalamu wa Veterinary Science),* Abdulghafur Hemed Al-Busaidy *(Mtaalamu wa Applied Physical Chemistry),* Alwy Mohamed Shatry *(Mtaalamu wa Veterinary Science), na* Rashid Mzee *(Mtaalamu wa Genetics)* walikuwa wakichangia Makala ya *Sayansi katika Kioo cha Qur'an* katika jarida la *Sauti ya Haki.*

Jambo jengine aliloliwekea umuhimu ni kuihifadhi lahaja ya Ki-Mvita ya lugha ya Kiswahili. Ingawa alianza kuandika kwa Kiswahili Sanifu. Alipotambua hatari ya kuweza kupotea lahaja hii, akabadilisha uwandishi na kutumia Ki-Mvita ili lahaja hii ihifadhike. Hii inaonyesha namna yalivyokuwa maoni yake ya mbali.

Sauti ya Haki ilikusanya mambo mengi:

- Mada juu ya mambo yanayotokea kila leo katika mujtamaa yafafanuliwe ili ijulikane Uislamu unasema nini juu ya jambo hilo.
- Tafsiri ya kitabu cha Sh. Al-Amin Mazrui kiitwacho *Hidayatul Atfal* – Uwongozi kwa Watoto. Kitabu hiki kimekusanya mafunzo ya dini kwa njia nyepesi ili mwanafunzi aweze kuifahamu dini yake juu ya mambo yanayo mlazimu.
- Kitabu cha Sh. Al-Amin cha *Al-Ahadithul Mukhtar – Hadithi zilizochaguliwa*. Sh. Muhammad akawa anazitia Hadithi moja moja na kuzisheresha ili zizidi kufahamika. Hiki ni kitabu kilichokusanya Hadithi fupi fupi 130 zinazofundisha mambo ya *Akhlaq* na mambo mepesi ya kuifahamu Dini. Masha'Allah kitabu hiki kimepata bahati, kinatumika katika Madrasa nyingi nchini kwani kimekusudiwa wanafunzi wa Madrasa.
- *Sayansi katika kioo cha Qur'an* – Ikieleza mambo ya ki-sayansi yaliotajwa ndani ya

Qur'an na kuyachambua kwa njia nyepesi ili yafahamike na mtu wa kawaida. Na pia kuwafunulia watu kuwa Qur'an imekusanya mambo tofauti tofauti, na kuwa Uislamu haupingani na Sayansi, bali Qur'an imetaja na kufafanua mambo hata kabla wana-Sayansi hawajayajua, wacha kuyafanyia utafiti. Mfano Qur'ani imeeleza elimu ya uzazi, *Embryology;* elimu ya Sayari, *Astronomy*, hesabu za aina mbali mbali kama elimu ya Mirathi; elimu ya Geographia, n.k.

- Maelezo juu ya Hadithi za *Arba'in Nawawy* – Hadithi 40 zilokusanywa na Imam Nawawy. Ikatajwa Hadithi moja moja, na kuitilia Sherehe ili Hadithi ifahamike zaidi.
- Fatawa – ikawa ni majibu ya maswali yanaoletwa na wasomaji mbali mbali wakitaka ufafanuzi juu ya matatizo yanayo wakabili, na nini hukumu za Kidini. Akapewa nafasi Sh. Abdalla Swaleh Farsy kuyajibu maswali hayo kwa njia ya Fatwa.
- Mkia wa Dhahabu – Ikieleza juu ya mambo ya dharura yanayo jitokeza yanayo hitaji maelezo marefu zaidi.
- Mara kwa mara mulikuwa mukitiwa mashairi mbali mbali yaliochangiwa na Washairi.
- Na kila mtaalamu alokuwa na kitu muhimu cha kuwafaa watu nae alikuwa akipewa nafasi ya kuchangia.

Usambazaji wa *Sauti Ya Haki*

Sauti ya Haki ilisambaa sana – Afrika Mashariki na nchi nyingi nyengine. Na kule ilikosambaa utakuona ukiyaangalia kule yanapotoka maswali. Mfano, tuchukue jarida No. 1/81 la tarehe 15 January 1981, Rabi-ul Awwal 1401 – maswali yalitoka Kwale, Lamu, Nakuru – Kenya; Kigoma, Mbeya, Morogoro, Ujiji, Pangani –Tanzania; na Dubai.

Sh. Muhammad Kassim alitumia njia mbali mbali za kuisambaza Sauti ya Haki:

— Shariff Yusuf Tamim Baalawy alikuwa ni mmoja katika watu walokuwa wakilisambaza jarida hili kwa wateja wake wengi. Na Masha'Allah alikuwa na mtandao wake mkubwa. Mkewe ni Bi. Aisha binti Sh. Al-Amin Mazrui. Hawa ndio wazazi wa Mwandishi wa kitabu hiki.

— Bw. Ismail Abdalla aliyekuwa karani wa Kadhi Mkuu wakati wa Sh. Abdalla Swaleh Farsy na Sh. Nassor Nahdy. Akachaguliwa kama Kadhi wa Eldoret, na baadae kuwa Kadhi wa Lamu. Bwana huyu alikuwa na mahusiano mazuri na Sh. Muhammad Kassim. Yeye ndiye aliyekuwa akiwatumia watu jarida hili kwa njia ya Posta. Kila aliyetaka apelekewe jarida hili, alikuwa akileta anwani yake. Kazi ya Ismaili ikawa ni kuwatumia kila linapotoka. Bwana Ismail ni

mzaliwa wa Changamwe, Mombasa, na amefariki akihudumu kama Kadhi wa Lamu.

— Katika kila mji alikuwepo mtu maalumu aliyekuwa akipelekewa majarida kadha, na yeye akawa ndiye msambazaji katika mji wake – Mombasa, Takaungu, Malindi, Lamu n.k.

Vitabu vya Sh. Muhammad Kassim Mazrui:

1. *Mirathi katika Sharia ya Kiislamu* – 1943 (1362 H). Sh. Muhammad Kassim alikiandika kitabu hiki pamoja na nduguye, Sh. Rashid Kassim. Kitabu kikapitiwa na kusahihishwa na Mwalimu wao, Sh. Al-Amin Mazrui.
2. *Uwongozi* – 1944 (1363 H). Huu ni mkusanyiko wa makala yaliochaguliwa kutoka katika magazeti ya *Sahifa* na *Al-Islah* yalokuwa yakiandikwa na kutolewa na Sh. Al-Amin Mazrui. Ukawa ni ushirikiano wa Sh. Muhammad Kassim na nduguye, Sh. Rashid Kassim. Dibaji ikaandikwa na Sh. Al-Amin.
3. *Maisha ya Assidik Abubakar* – 1958 (1377 H). Baada ya Sh. Abdalla Swaleh Farsy kuandika juu ya Maisha ya Mtume Muhammad (S.A.W.), Sh. Muhammad akatamani na yeye aimalizie Serah hiyo tukufu kwa kuandika juu ya Makhalifa wane. Hiki kikiwa ni juu ya Khalifa wa kwanza wa Mtume (S.A.W.). Sayyidna Abubakar akiwa

ni mfuasi, rafiki na mkwe wa Mtume. Binti yake, Bibi Aisha akiwa ni mmoja kati ya wake wa Mtume (S.A.W.) – *Ummahatul Muu'mineen*.

4. *Maisha ya Al-Faruk Umar* – 1962 (1381 H). Huyu ni Khalifa wa pili. Nae akawa mfuasi shupavu na mkwe wa Mtume (S.A.W.). Binti yake, Bibi Hafsa, akiwa miongoni mwa *Umahatul Muu'mineen*.
5. *Maisha ya Dhin-Nurain Uthman* – 1964 (1383 H). Huyu ni Khalifa wa tatu. Alipata bahati ya kuwaoa binti wawili wa Mtume (S.A.W.) – Bi. Ruqayya na Bi. Zeinab binti Rasuli Llah.
6. *Maisha ya Imam Ali* – 1965 (1384 H). Huyu ni Khalifa wa nne, nae akapata bahati ya kumuoa Bibi Fatmah binti Rasuli Llah. Kitabu hiki kilifichua mambo mengi ambayo watu wakidhani ndiyo misimamo ya kidini, kumbe zilikuwa ni njama tu za kuwahadaa watu. Wale walokuwa wakifanya njama hizo wakazua mjadala mkubwa sana kwa kufichuliwa hadaa zao.
7. *Historia ya Utumwa katika Uislamu na Dini nyengine* – 1970 (1390). Kitabu hiki kinaonyesha mahusiano baina ya Mwalimu, Sh. Al-Amin, na Mwanafunzi wake, Sh. Muhammad Kassim. Hapa tunanukuu kutoka kwa Dibaji ya kitabu hicho:

   Aliyekusudia kuandika kitabu hiki mbele ni mwongozi wetu maarufu Kadhi Mkuu wa

zamani, marehemu Sheikh Al-Amin bin Ali, wakati alipoona maneno yaliyotangazwa katika ***Habari*** *(No. 61 ya 5/9/1946, uk. 8) kuhusu UTUMWA na WAARABU. Likisema gazeti hilo – bila ya muktadha wala mnasaba wowote ila kusudi ya kutukana na kutia chuki baina ya Waislamu na wasiokuwa Waislamu, na baina ya Waarabu na wasiokuwa Waarabu.*

Kitabu alichokusudia kuandika alikipa jina hili "Utumwa katika Dini na Mataifa ya Ulimwenguni". Na akapanga mpango wa yale aliyokusudia kuandika, kama ilivyokuwa desturi yake. Kwa bahati mbaya kwa Waislamu, na kwa bahati nzuri kwa Wakristo, akapata ugonjwa na kufariki dunia kabla ya kuanza kazi yake. Mungu Amrehemu.

..... Ndipo nilipokusudia mimi, mmoja katika wanafunzi wa marehemu huyo, kusimama kwa kazi hiyo, na kuandika juu ya yale aliyokusudia mwenyewe katika mpango wake. Makusudio yangu kwa kazi hii ni kuitumikia dini yangu ya haki na kumtumikia Sheikh wangu.

8. *Hukumu za Sharia* – Sehemu ya I, II na III – 1970/1971 (1390/1391 H) ikifafanua mada moja juu ya nyengine kulingana na hukumu za Sharia.

9. *Sitara ya Wanawake* – juu ya mambo muhimu yanayo wahusu wanawake na sitara yao katika mujtamaa.
10. Gazeti la *Sauti ya Haki* – 1972-1982 (1392-1402 H). Likitolewa kila baada ya miezi mitatu kwa muda wa hiyo miaka kumi. Maelezo zaidi baadae.
11. *Tafsiri ya Qur'ani Tukufu: Al-Faatihah – Al Baqarah* – 1980 (1400 H). Ameiendeleza Tafsiri ya Qur'ani ya Mwalimu wake, Sh. Al-Amin b. Ali Mazrui. Mwalimu alifasiri na kutia maelezo hadi kufikia Al-Baqarah Aya ya 160. Akaendelea kufasiri bila ya maelezo mpaka Aali Imran Aya ya 170. Maelezo zaidi baadae.
12. *Tafsiri ya Qur'ani Tukufu: Aali Imraan – An-Nisaa"* – 1981 (1401 H). Akiendeleza Tafsiri ya Qur'ani ya Mwalimu wake, Sh. Al-Amin b. Ali Mazrui. Na yeye akaifikisha mpaka mwisho wa Al-Hijri. Hapo akasallim amri ya *Malakul maut* na kuiaga dunia.

Walio shughulika katika kazi ya uwandishi

Sh. Muhammad Kassim aliazimia kuiendeleza Tafsiri ya Sh. Al-Amin baada ya kustaafu kwake kama Kadhi Mkuu wa Kenya.

Kwa bahati mbaya alipostaafu alipata ugonjwa wa macho, ikawa hawezi kusoma wala kuandika. Baada ya miaka kumi na moja, wanawe, Bw. Munir, Profesa Alamin na Sh. Hammad, wakajitokeza na

kumuhimiza baba yao na kujitolea kumsaidia kwa kila njia, ili aweze kuitimiza azma yake. Ikawa kila wanapopata nafasi hukaa na baba yao na kumuandikia. Na kwa bahati nzuri, Abdalla Muhammad Awadh alipomaliza kusoma sekondari, akaombwa aifanye yeye kazi hiyo. Ikawa Abdalla ana nafasi na umakinifu wa kukaa na Sh. Muhammad Kassim kwa masaa marefu zaidi, takriban masaa matatu kila siku kutoka Jumatatu hadi Ijumaa ya kila wiki.

Mwengine aliyetumika mara kwa mara katika usaidizi wa kuandika *Sauti ya Haki* na vitabu ni wanawe wengine, Bi. Hafidah, Bi. Layla na Bi. Sauda. Na mara moja moja Bw. Ahmad Muhammad Ali Mandhry.

Mwengine pia aliyejitolea katika kazi hii ni Bi. Faiza Mazrui. Alhamdu Lillah! Sh. Muhammad amewataja mwenyewe wasaidizi wake katika Dibaji ya Tafsir. Allah awalipe kila la kheri kila aliyesaidia, wale walotajwa na ambao hawakutajwa, kwa jitihada yao hii ya kusaidia katika uwandishi – Ameen.

Mwelekeo wa Tafsiri

Sh. Muhammad Kassim na Sh. Abdalla Swaleh Farsy walipokea *Tafsiri ya Jalaleyn* kutoka kwa Mwalimu wao, Sh. Al-Amin Mazrui. Wote wakachukua jukumu la kuifasiri Qur'ani kwa Kiswahili.

Sh. Muhammad Kassim akaendeleza Tafsiri ya Sh. Al-Amin kwa mwelekeo mmoja, na Sh. Abdalla akauchukua mwelekeo mwengine. Sh. Muhammad akaendeleza jihadi ya kupigana vita vya aina moja, nae Sh. Abdalla akaendeleza jihadi ya kupigana na Makadiani (Ahmadiya).

Moja katika malengo ya kwanza ya Tafsiri ya Sh. Al-Amin ilikuwa ni kuirudi na kuisahihisha tafsiri bandia ya Padri Dale. Baadae ikachukua mwelekeo mpana zaidi wa kuwawekea wazi kwa njia rahisi, mafunzo yanayo patikana katika Qur'ani. Na kwa sababu hii, kila yanapo hitajika maelezo marefu zaidi, Sh. Muhammad aliyapanua maelezo hayo. Kwa mfano:

1. Katika mwisho wa Tafsiri ya Al-Baqarah ametia ukurasa wa 135-145 kijalizo cha bishara kumi zilizomo katika vitabu vya Wamasihia na Mayahudi juu ya Mtume Muhammad (S.A.W.). Bishara kumi hizi zikiwa ni Makala yaliomo katika kitabu cha Sh. Al-Amin alichokiandika 1939, nikinukuu: *Dini Ya Islamu – Kimekusanya ushuhuda wa watu wa Ulaya kwa Dini ya Isilamu, maneno ya vitabu vitakatifu kwa Mtume Muhammad, mafundisho ya Dini ya Isilamu, hisabu ya Waisilamu waliyo Ulimwenguni hivi leo.*
2. Katika mwisho wa Tafsiri ya An-Nisaa, amekinukuu kitabu cha Sh. Muhammad na Sh. Rashid Kassim Mazrui kilichoandikwa

1943 (1362 H), *Mirathi katika Sharia ya Ki-Islamu*. Yakiwa ni maelezo na mafundisho kamili juu ya Mirathi na namna ya kuwagawanyia wale wanaofaa kurithi mali yalioachwa na jamaa zao.

Kwa hivyo Tafsiri hii ina malengo mapana zaidi juu ya mambo yanayo hitajika kujulikana na Mujtamaa.

Moja katika Ayah za mwisho alizozifasiri Sh. Muhammad Kassim kabla ya kufa ni Al-Hijri 15:99,

15:99 Na muabudu Mola wako mpaka ikufikie Yakini [yakufikie mauti].

Hii ikiwa ni Ayah ya mwisho ya Surah Al-Hijri. Sh. Muhammad ameutumikia Ummah mpaka mwisho wa maisha yake. Ayah hii ameifasiri siku ya Ijumaa ya tarehe 2 Aprili 1982 (7 Jumadal Akhira 1402), na kufariki asubuhi mapema ya Jumatatu tarehe 5 Aprili 1982 (10 Jumadal Akhira 1402). Allah amemuwafikia kuimalizia kazi yake ya kuifasiri Qur'ani kwa bishara hii ya kumtumikia na kumuabudu Mola wake mpaka yalipomfikia mauti.

Jumatatu asubuhi, Abdalla alikuwa ameanza safari ya kwenda Kisauni kwa Sh. Muhammad Kassim ili waendelee na kazi hii ya Tafsiri. Njiani anakutana na Al-Akh Munir Muhammad Kassim Mazrui ambae alimpa khabari kuwa baba amefariki

asubuhi hiyo – *Inna Lillahi wa inna Ilaihi rajiun!* (Hakika sisi tunatoka kwa Mwenye-ezi-Mngu, na kwa hakika tutarudi Kwake).

Hivi ndivyo alivyo kadiriwa Sh. Muhammad Kassim Mazrui katika kazi hii tukufu ya kuufahamisha Ummah nini mafunzo ya Dini yao. Tunamuomba Allah aibariki kazi yake hii, iwe ndiyo sababu ya kuipata Jannatul Firdaus, In shaa Allah – Ameen.

Kwa hivyo Tafsiri aloianzisha Sh. Al-Amin Mazrui iliendelezwa na Mwanafunzi wake mkubwa, Sh. Muhammad Kassim Mazrui. Sh. Al-Amin alimaliza kuitafsiri Aya ya *A'ali Imran* 3:170 kabla ya kufa kwake. Tafsiri na maelezo yake alikoma katika Surah Al-Baqarah 2:160, na kuendelea mpaka 3:170 bila ya maelezo. Jukumu hilo likamuangukia Sh. Muhammad Kassim. Yeye akajaliza maelezo na Tafsiri mpaka mwisho wa Surah An-Nisaa 4:176. Akafanya bidii kuzichapisha Tafsiri hizo katika vitabu viwili, cha kwanza ikiwa ni cha *Surah Al-Faatiha na Al-Baqarah*, na cha pili kikiwa ni *Surah A'ali Imran na An-Nisaa*. Vyote viwili akavichapisha na kuvitoa kwa jina la Mwalimu wake, Sh. Al-Amin.

Hapa ninamnukuu Sh. Muhammad Kassim Mazrui katika maelezo aliyo yaandika juu ya tafsiri ya Sh. Al-Amin katika Dibaji ya *Tafsiri ya Qur'ani Tukufu: Al-Faatihah-Al-Baqarah:*

Sheikh aliandika Tafsiri hii katika mwaka wa 1936 kwa azma ya kuikamilisha na kuipamba kwa maelezo yake.....

Wakati Sheikh Al-Amin alipokuwa akiendelea na kazi hii kwa hima kubwa, alifika Mombasa mwanachuoni mmoja mashuhuri, Sheikh Muhammad bin Abdil-Alim As-Siddiq. Walipoonana, mwanachuoni huyo alimuuliza shekhe wetu kama anayo azma ya kufasiri Qur'ani kwa lugha ya Kiswahili. Sheikh akamjibu kuwa ashaanza kazi hiyo, na akamtajia kuwa sababu moja iliyompa kufanya kazi hiyo ni kumrudi Padri Dale. Sheikh Muhammad bin Abdil-Alim asimwafiki katika hiyo azma yake, akamwambia: "Dale ajulikana kuwa ni padri wa Kikristo. Kwa hivyo hapana Islamu yoyote atakayeshughulika na kuisoma tafsiri yake. Lakini utakapoirudi itakubidi unakili maneno yake, uyatie katika tafsiri yako ili upate kuyavunja. Hapo maneno ya Dale na upotofu wake yatawafikilia Islamu kwa wasita wa tafsiri yako. Na humjui ni yupi atakaeathirika kwa maneno yake." Nasaha hii ilimwathiri sana shekhe wetu, na ikamtepeteza na kuendelea na kazi yake. Hapo alikuwa amekamilisha maelezo ya Ayah ya 160 ya Al-Baqarah, na tangu wakati huo akaendelea na tasiri bila ya maelezo, na huku akitaradadi baina ya kufwata nasaha ya Sheikh Muhammad Abdil-Alim na kutoifwata.

Sh. Al-Amin wakati wa uhai wake, aliweza kuchapisha Tafsiri ya Juzuu ya Ammah. Kazi ilobaki sasa ni kuchapisha Surah ya nne hadi Surah ya 15. Tunataraji wanawe, khasa Sh. Hammad ataweza kuiendeza kazi hii tukufu ya babaake. Kama alivyo fuata khatua za babaake katika kazi za Ukadhi na Darasa za Wazee na za kina mama, tunataraji pia atafuata khatua hizi za kuimaliza Tafsiri ya Qur'ani. In shaa Allah, Mwenye-ezi-Mngu amtilie tawfiki, Amin.

Ama mwanafunzi mwengine wa Sh. Al-Amin, nae ni Sh. Abdallah Swaleh Farsy yeye aliweza kuimaliza na kuchapisha Tasiri kamili kama *Qurani Takatifu*. Sh. Abdalla vile vile akaendeleza jihadi ya kupambana na Makadiani aloianza Sh. Al-Amin. Wanafunzi hawa wawili, Alhamdu Lillah, wamefuata khatua za Mwalimu wao za kuutumikia na kuuamsha Ummah waweze kuifahamu Dini yao vilivyo. Allah awalipe mema wote watatu, Mwalimu na Wanafunzi wake, awajaalie, In shaa Allah, ni watu wa Jannatul Firdaus, Amin.

Mahusiano baina ya Sh. Muhammad Kassim Mazrui na Sh. Al-Amin b. Ali Mazrui

Sh. Muhammad Kassim ni binamu wa Sh. Al-Amin kama tulivyo tangulia kusema katika utangulizi.

Mbali na uhusiano huu wa kidamu, kubwa zaidi ni kuwa Sh. Muhammad Kassim amelelewa na kusomeshwa na Sh. Al-Amin. Yeye akiwa ni mmoja katika wanafunzi na wafuasi (*Disciple*) wa Sh. Al-

Amin. Katika jumla ya elimu alizosoma kutoka kwa Sh. Al-Amin ni Tafsiri ya Jalalein kama alivyopokea Sh. Abdalla Swaleh Farsy (angalia Silsila zao katika Tafsiri zilizo chapishwa).

Sh. Muhammad pia alikuwa msaidizi mkubwa katika kazi za Sh. Al-Amin. Yeye ndiye aliyekuwa akizichapisha jarida la *Al-Islah* na *Sahifa*. Pia alikuwa akitumwa sehemu mbali mbali kila panapokuwa na dharura.

Yeye ndiye aliyekuwa msitari wa mbele wakati alipokufa Sh. Al-Amin, akayasimamia mazishi ya Shekhe wake kwa kila lililohitajika. Ikawa yeye ndiye aliyezirithi kazi zake, na kumtimizia yale aliyousia afanyiwe.

Sh. Al-Amin akamuozesha Sh. Muhammad Kassim binti yake wa kwanza, Bi. Salma binti Sh. Al-Amin Mazrui. Huyu ndiye mama wa Bw. Munir, Bi. Maimuna, Profesa Alamin na Bi. Hafidah.

Watoto wengine wa Sh. Muhammad Kassim ni Sh. Hammad, Bw. Gharib (wa MEWA), Bi. Layla na Bi. Sauda.

Sh. Muhammad Kassim kama Mshairi

Sh. Muhammad Kassim kama alivyokuwa Mwalimu wake, Sh. Al-Amin Mazrui, alikuwa hodari wa kutunga Mashairi. Ameandika mashairi mengi yakiwemo yale ya matayarisho ya mauti yake, akiwaaga na kuwausia jamaa zake pamoja na

Mujtamaa. Mashairi hayo yalisomwa na binti yake, Bi. Maimuna, kabla ya maiti kutolewa nyumbani.

Hapa nanukuu baadhi ya tenzi hizo za kuaga zilizochapishwa katika *Sauti ya Haki* jarida No.2/82, likiwa na kichwa, *Muhariri Wetu Aaga Dunia:*

Haya hayana haula Wala quwata
Wala hayana muhula Yakifisha hukupata

Pindi neema ya Mola Ikitaka kukuwata
Ajali hukufuwata Huna pa kukimbilia

Kati ya mashairi yake yaliyo wahi kuchapishwa ni yale aliyomtungia Sh. Abdalla Swaleh Farsy akimpongeza wakati alipochaguliwa kama Kadhi Mkuu wa Kenya 1968 (1388 H), na mengine ya kuipongeza *Tafsiri ya Qur'ani Takatifu.*

Urafiki wa Sh. Muhammad Kassim Mazrui na Sh. Abdalla Swaleh Farsy

Baada ya kustaafu kwa Sh. Muhammad Kassim kama Kadhi Mkuu wa Kenya 30 April 1968 (2 Safar 1388), Sh. Abdalla Swaleh Farsy ndiye aliyechaguliwa kuichukua nafasi hiyo. Tarehe ya Ma-Ulamaa wawili hawa ni madrasa kamili inayofaa kutungiwa vitabu.

Ajabu ya kwanza ya marafiki hawa ni kuwa wamezaliwa mwaka mmoja, na kufariki mwaka mmoja – 1912-1982 (1330-1402). Sh. Abdalla alipostaafu mwaka wa 1980 (1400 H) alihamia

Muscat kujiunga na familia yake. Alipopelekewa habari za kufariki kwa Sh. Muhammad alisikika akisema na mimi pia nimeshakufa. Na kweli baada ya miezi kadha na yeye pia akaaga dunia kama alivyotabiri. Na hii ndio kawaida ya watu waloshibana sana. Mfano mwengine mzuri ni ule wa Sayyid Ahmad Bin Sumeyt na Sh. Abdalla Bakathiri – 1861-1925 (1276-1343 H).

Sh. Muhammad na Sh. Abdalla kwanza walijuana Unguja wakati Sh. Muhammad alipopelekwa Zanzibar na Mwalimu wake. Baadae Sh. Abdalla alikuja Mombasa kusoma *Tafsiri ya Jalaleyn* kwa Sh. Al-Amin. Sh. Abdalla kwanza aliisoma *Tafsiri ya Jalaleyn* kwa Sh. Ahmad Muhammad Mlomry, Mwanafunzi wa Sh. Ali b. Abdalla Naf'i. Hapo tena urafiki wa Ma-Ulamaa hawa wawili, Sh. Muhammad na Sh. Abdalla, ukazidi kukuwa na kujengeka. Wote wawili walikuwa wanafunzi wakubwa wa Sh. Al-Amin Mazrui. Urafiki wa dhati ulojengwa juu ya misingi ya Imani na Taqwa, urafiki wa mahaba makubwa, urafiki wa kukinaiana. Wakajenga urafiki baina yao, na baina ya familia zao.

Marafiki hawa wakawa ni washauri wakubwa baina yao. Wakishauriana juu ya mambo mbali mbali katika makazi na kuutumikia kwao Mujtamaa. Darasa za Misikiti alizokuwa akisomesha Sh. Muhammad akamrithisha Sh. Abdalla.

Sh. Abdalla akaweza kumpokea Sh. Muhammad baada ya kustaafu kwake. Nae Sh. Muhammad akawa ni Mshauri mkubwa wa Sh. Abdalla katika kazi zake za U-Kadhi Mkuu na kwa mengi mengineo. Alhamdu Lillah! Ma-Ulamaa hawa wawili wakawa ni *Lujna* kamili. Mujtamaa ukafaidika kwa kuwepo kwao, wakaweza kuyatatua mambo mengi yalokuwa yakiwakabili watu. Mwenye-ezi-Mngu awalipe kwa kazi yao kubwa walioifanya katika kuitumikia dini yao na kuuelimisha Ummah.

Tujifunze nini kutoka kwa nafasi tunu aloipata Al-Akh Abdalla Muhammad Awadh kwa kumtumikia Sh. Muhammad Kassim Mazrui katika kazi ya kuutumikia Mujtamaa wetu?

Kukaa na Mwanachuoni ni Madrasa kubwa, utasoma mengi ambayo si rahisi kuyapata katika darasa la kawaida. Uzione khulka na tabiya zao, fikra na maoni yao, ushujaa na uadilifu wao, ukarimu na Ucha-Mngu wao, kipawa cha elimu na mizani yao yakupimia mambo yanayo jitokeza kila leo katika Mujtamaa. Na uwaone namna wanavyoichunga heshima yao.

- Haiba na utisho: Sh. Muhammad Kassim Mazrui alikuwa na haiba na utisho. Lakini la ajabu ni kuwa ukikaa nae, mara moja utamzoea, akupe nafasi ya kuzungamza nae bila ya khofu.

- Mausio kwa wazee: Watoto wako wakiwa wakubwa (kwa umri), basi wafanye marafiki – yaani usiamiliane nao kama watoto, bali amiliana nao kama marafiki.
- Kuchunga wakati: Juu ya hali yake kiafya na kiumri, aliutumia wakati wake kuutumikia Ummah mpaka mwisho wa maisha yake. Na katika vikao baina ya Sh. Muhammad na Al-Akh Abdalla, Sheikh hakutoka katika maudhui. Ikawa anautumia wakati huo kwa lile lengo lililo wakutanisha – la kuiandika Tafsiri ya Qur'ani. Mazungumzo yao yakawa kwenye mada hiyo na kuutumia wakati kwa kusudio hilo.

Sh. Ali b. Abdalla Naf'i (1825-1894)

Sh. Al-Amin b. Ali (1891-1947)

Sh. Muhammad K. Mazrui & Sh. Abdalla S. Farsy (Wote 1912-1982)

Sh. Muhammad K. Mazrui & Sh. Abdalla S. Farsy
(Wote 1912-1982)

Liwali Salim M. Muhashamy (1911-1979)

Ustadh Harith Swaleh (Amezaliwa 1937)

1980 - Baraza la Wazee wa kimji lakutana nyumbani kwa Sh. Muhammad Kassim Mazrui, Mwandoni, Kisauni. Hii ikiwa ni moja katika hafla zilizofanywa za kumuaga Sh. Abdalla Swaleh Farsy.

Liwalis, Mudirs and Kadhis At Government House Mombasa 1958

From left: Sh. Rashid AlRiyami-- Sh.Mohamed S. Qassim-- Sh. Ali Mohamed(Qadhi)-
Sh.Ahmed A. Yusuf--Sh. Abdullah Bafadhil(Qadhi)--Sh. Masoud Ali Muhashamy--
Sh.Mohamed Jawad-- Sh. Abdullah M. Al Mandhry-- Sh. Harith A. Al Mazrou--
Sh. Abdullah M. Khatib
Sitting: Sh. Mammun Al Mazru (Qadhi) -- Sh. Rashid Azzan Al Suqri(Liwali)--
Sh. Salim Al Muhashamy (Liwali)-- Sh. Sir. Mubarak Ali Al Hinawy KBE (Liwali for the Coast)
Sh. Al Amin Al Mandhry (Liwali) -- Sh. Mohamed Al Qamshu (Liwali)--
Sh. Mohamed Q. Al Mazrui (Cheaf Qadhi)

GOVERMENT HOUSE DECEMBER 1958 - MOMBASA KENYA

Bibliography

1. *Abdalla Muhammad Awadh* - Majadiliano katika Msikiti wa Mazrui, tarehe 29 April 2018
2. *Sh. Muhammad Kassim Mazru* - **Sauti ya Haki, toleo la No. 2/82 la 1 May 1982**
3. *Sh. Muhammad Kassim Mazrui* - **Historia ya Utumwa katika Uislamu na Dini Nyengine**
4. *Ma-Profesa Kai Kresse & Hassan Mwakimako* – **Guidance (Uwongozi) by Sheikh Al-Amin Mazrui: Selections from the First Swahili Islamic Newspaper – A Swahili_English Edition**
5. *Profesa Kai Kresse* - **'Swahili Enlightenment? East African Reformist Discourse At The Turning Point: The Example Of Sheikh Muhammad Kassim Mazrui**
6. *Sheikh Al*-Amin Bin Ali Mazrui – **Tafsiri ya Qur'ani Tukufu: Al-Faatihah-Al-Baqarah**
7. *Sh.* Abdalla Swaleh Farsy – **Baadhi ya Wanavyuoni wa KiShafi wa Mashariki ya Afrika**
8. *Ghalib Yusuf Tamim* – **Maisha ya Sh. Muhammad Kassim Al-Maamiry**
9. *Ustadh Harith Swaleh* – Majadiliano nyumbani kwake, Mjuakale, Mombasa